**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUMU**
**CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII TENGERU**

# TANGAZO LA ZABUNI YA UPANGISHAJI WA MAJENGO/ VYUMBA VYA BIASHARA

**TAREHE: 29/8/2024**

1. Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru inawatangazia makampuni,watu binafsi, vikundi na Taasisi zilizosajiliwa na kuendeshwa kwa mujibu wa sheria , kanuni na taratibu za nchi, nafasi za kupanga vyumba vya biashara/mgahawa wa wanafunzi na 'canteen' ya watumishi katika majengo ya chuo kwa ajili ya kufanya biashara.
2. Tangazo hili linatolewa kwa muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe 29/08/2024 hadi tarehe 11/09/2024 ili waombaji wenye nia na sifa kuweza kutuma maombi yao.
3. Mchanganuo wa zabuni zinazotangazwa umeoneshwa katika jedwali hapa chini:-

| NA | ZABUNI | NAMBA YA ZABUNI | ENEO ILIPO /JENGO |
|---|---|---|---|
| 1 | Ukodishaji wa 'cafeteria' ya wanafunzi | TR25/2024/2025/HQ/NC/01 | STUDENT CAFTERIA |
| 2 | Ukodishaji wa canteen | TR25/2024/2025/HQ/NC/02 | STAFF CANTEEN |
| 3 | Ukodishaji wa chumba cha 'stationery' | TR25/2024/2025/HQ/NC/03 | 4A – BLUE HOUSE |
| 4 | Ukodishaji wa chumba cha 'stationery' | TR25/2024/2025/HQ/NC/04 | 4B – BLUE HOUSE |
| 5 | Ukodishaji wa chumba cha 'stationery' | TR25/2024/2025/HQ/NC/05 | 4C - BLUE HOUSE |
| 6 | Ukodishaji wa chumba cha 'stationery' | TR25/2024/2025/HQ/NC/06 | 4D- MKWAWA |
| 7 | Ukodishaji wa chumba cha 'stationery' | TR25/2024/2025/HQ/NC/07 | 4E–STUDENT CAFTERIA |
| 8 | Ukodishaji wa chumba cha 'stationery' | TR25/2024/2025/HQ/NC/08 | STAFF CANTEEN |
| 9 | Ukodishaji wa chumba cha 'stationery' | TR25/2024/2025/TWN/NC/09 | KITUO CHA MJINI (KIJENGE-MWANAMA) |
| 10 | Ukodishaji wa chumba | TR25/2024/2025/HQ/NC/10 | KIBANDA CHA MAJI |
| 11 | Ukodishaji wa chumba cha Saloon ya Kike - Bweni la Samia | TR25/2024/2025/HQ/NC/11 | SAMIA HOSTEL |
| 12 | Ukodishaji wa chumba cha 'stationery' –Bweni la Samia | TR25/2024/2025/HQ/NC/12 | SAMIA HOSTEL |

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WA ZABUNI YA UPANGAJI**

1. Zabuni zinatangazwa kwa makampuni, watu binafsi, vikundi na Taasisi zenye sifa, nia na uwezo wa kupanga vyumba kwa ajili ya biashara.

   ***NB: Sheria ya Ununuzi ya Umma namba 10 ya Mwaka 2023 kifungu namba 108(1), (3) na (5) Kinakataza kiongozi au Mtumishi wa umma au ndugu kujihusisha na zabuni.***

2. Ada ya maombi ya zabuni ni shilingi hamsini elfu (Sh.50, 000.00) kwa kila zabuni na haitarejeshwa iwapo utakosa Zabuni husika

3. Nyaraka za zabuni zinapatikana katika **OFISI YA KITENGO CHA UNUNUZI NA UGAVI – TAASISI YA MAENDELEO YA JAMII TENGERU, S.L.P 1006, ARUSHA,** kila siku kuanzia saa 2.30 asubuhi hadi saa 9:30 mchana, siku za Jumatatu hadi Ijumaa [kuondoa siku za sikukuu zinazotambulika Kitaifa].

4. Ada ya zabuni na kodi ya Pango zitalipwa kwa kutumia Namba ya malipo '**Control Number'** itakayotolewa na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Ili kupata Namba ya Malipo tafadhali, wasiliana na Mhasibu wa mapato, CPA NASSORO MSHANGAMA, Simu **0712 464,172**.

5. Mwombaji anaruhusiwa kutembelea vyumba na migahawa inayopangishwa kabla ya kujaza zabuni, siku zote kuanzia tarehe ya tangazo hili hadi siku ya mwisho, muda kuanzia saa 2.00 hadi 9.30 kwa siku za kazi tu.

6. Mwombaji baada ya kuona na kuchagua chumba/mgahawa, **ajaze bei/gharama** ya pango anatakayopenda kulipa katika fomu ya gharama iliyopo katika kabrasha la zabuni.

7. Mwombaji aliyekuwepo awali na anapenda kuendelea kuwa mpangaji atapewa kipaumbele endapo atakuwa Hadaiwi kodi ya Pango na amekidhi vigezo vyote vya zabuni.

8. Mwombaji aambatishe Stakabadhi ya ada ya zabuni; Leseni halali ya biashara na hai, pia, Namba ya Usajili wa mlipa kodi (TIN/VAT), cheti cha TMDA kwa migahawa na Tamko dhidi ya vitendo vya Rushwa.

9. Mwombaji asiombe zabuni na kupangisha mtu mwingine.

10. Kwa waombaji wa mgahawa wa wanafunzi na canteen ya watumishi, waambatishe **MCHANGANUO AU MENU YA CHAKULA INAYOONESHA BEI ZA VYAKULA**, ikizingatiwa kuwa Taasisi inahudumia wanafunzi na watumishi wa hali zote.

11. Mikataba yote itadumu kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia tarehe 01 oktoba, 2024 hadi 01 oktoba , 2029 na itafanyiwa mapitio kila mwaka, ambapo mpangaji ambaye atashindwa kutekeleza makubaliano ya mkataba katika mwaka husika, ataondolewa na kupewa mpangaji mwingine atakaye kuwa tayari kufuata masharti ya mkataba.

12. Mwombaji atakayekidhi vigezo vya mkataba na ana nia ya kupanga atatakiwa kulipia kodi ya pango la miezi mitatu (3) kabla ya kusaini mkataba.

13. Maombi yote yafungwe kwa lakiri na bahasha juu iandikwe namba ya Zabuni na kuiwasilisha kwa Mkuu waTaasisi, Ofisi ya Kitengo cha Ununuzi na Ugavi, S.L.P 1006, Arusha, kabla ya tarehe 11/9/2024 saa 5.00 asubuhi.

***Juu ya bahasha iandikwe namba ya zabuni na anuani ifuatayo**:-*

**MKUU WA TAASISI,**
**TAASISI YA MAENDELEO YA JAMII TENGERU**
**S.L.P 1006,**
**ARUSHA**

14. Mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ni **saa tano (5) kamili asubuhi** (saa ya Afrika Mashariki) ya tarehe **11/09/2024** siku ya Jumatano**.**

15. Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa kushuhudia ufunguzi. Ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni mbele ya waombaji au wawakilishi wa waombaji waliochagua kuhudhuria ufunguzi huo utakaofanyika katika Ukumbi wa DR ROSAMARIE MWAIPOPO (EXTENSION).

16. Uongozi haulazimiki kumchagua mzabuni yoyote. Aidha, wazabuni au mpangaji yeyote ambaye alipewa chumba/mgahawa miaka iliyopita na akashindwa kutekeleza matakwa ya mkataba ikalazimu uvunjaji wa mkataba kati ya Taasisi na Mzabuni/mpangaji, hataruhusiwa kuomba zabuni.

17. Maombi yatakayo wasilishwa baada ya muda uliopangwa kuisha hayatapokelewa na hayatafunguliwa.

**Janeth I. Zemba**
**Kny: MKUU WA TAASISI**

Kny: MKUU WA TAASISI
TAASISI YA MAENDELEO YA JAMII
TENGERU
S.L.P. 1006
ARUSHA